# JARIDA LA ATD DUNIA YA NNE TANZANIA | Agosti 2017

"Popote pale wanaume kwa wanawake wanapolazimika kuishi katika maisha ya umaskini uliokithiri, haki za binadamu hukiukwa. Sote ni wajibu wetu wa dhati kujiunga pamoja na kuhakikisha kwamba haki hizi zinaheshimika". - Joseph Wresinski (1917-1988), founder of ATD Fourth World -

## Tahariri



"Hatuna budi kufanya kazi wote kwa pamoja ili kuhakikisha wale waanaoishi katika umasikini uliokithiri wanapata haki zao, sauti zao zinasikika na kuheshimiwa utu wao.". Magdalena Sepulveda Carmona, Mwandishi wa makala yanayohusu umasikini uliokithiri na haki za bindamau kutoka umoja wa mataifa.

Kwa kusimama na kupaza sauti iwe katika mikutano ya jamii au katika vikao vya umoja wa mataifa kila mwanajumuiya wa ATD anasimama na kuwatetea watu wanaoishi katika umasikini uliokithiri. Msimamo huu unahitaji ujasiri.

Padre Mtakatifu Joseph, Mwanzilishi wa ATD Dunia ya nne alizungumzia kuhusu marafiki wa kwanza wa ATD"Utu huu pengine mwanzoni walifikiri watajihusisha na programu za kawaida. Kwa kweli mwishoni walijikuta wanahatarisha uaminifu wao. Si tu walikuwa wanatetea idadi ya watu isiowezekana kutetewa lakini pia kupitia mipango yao walikua wakiyahukumu kimakosa mashirika ya misaada. Walikuwa na wasiwasi wa kuhatarisha uaminifu wao kwa hali hii wakiwa machoni pa watu wao wenyewe.

Katika jarida hili tutasikia mapendekezo ya mpango wa utetezi wa ATD elimu kwa wote. Timu ya elimu kwa wote imekutana na wadau wa elimu zaidi ya 1000 wakiwemo wazazi na Viongozi wa serikali za mitaa kwa pamoja waliwezesha majadiliano baina yao juu ya mada ya elimu kwa wote. Wanachama wa ATD pia walikutana na Afisa Elimu wa wilaya ya Ilala na alikubali kuongeza mapendekezo katika kazi yao.

Utafiti wa "kipimo cha umasikini" ulizinduliwa rasmi. Tunasikia kutoka kwa Bwana Kassian, mwanachana wa kamati ya Kitaifa ya utafiti inayoongoza mradi . Na mwisho kabisa Pelagie, rafiki mpya wa harakati hii akishirikiana mawazo yake katika kugundua ATD.
Kila mtu katika jarida hili yuko tayari kutetea haki za wale wanaoishi katika umasikini uliokithiri, Kupaza sauti kupinga udhalimu, kuhatarisha undugu na urafiki mbele ya jamii na marafiki zao kwa ajili ya wale wale wanaoishi katika umasikini uliokithiri. Kuweka msimamo kwa lengo la mabadiliko ya jamii . Kwa kupitia kila mpango wanajenga harakati zetu.

Hamisi Mpana
Mwanaharakati wa kudumu wa ATD.

**"Ni muhimu walimu na wazazi kukutana na kuwepo mawasiliano ya mara kwa mara ili kujua matatizo, mienendo na maendeleo ya mtoto wetu." - Mzazi.**

Baada ya kipindi cha utafiti timu ya elimu kwa wote ya ATD Dunia ya Nne kufanya utafiti na kukamilisha kwa kupata ripoti kamili. Timu iliweza kukutana tena kwa pamoja na kufikiria nini cha kuendelea kwa kipindi kijacho.

Ndipo likapatikana wazo la kusambaza matokea ya utafiti kwa kuyafikia makundi tofauti tofauti kwa njia ya mikutano wakiwemo watunga sera, maafisa elimu, viongozi wa serikali za mitaa na mikutano ya wazi mashuleni ambayo inayowakusanya walimu, wazazi na viongozi wa serikali za mitaa katika baadhi ya wilaya zilizopo ndani ya mkoa wa Dar es Salaam na hata nje ya mkoa. Kwa kufuata taratibu za nchi kwa kuweza kupata vibali na ruksa ya kuweza kufanya mikutano hii.

Lengo ni kuongeza uelewa kati ya wazazi, walimu na wanataaluma, viongozi wa mitaa na taasisi katika umuhimu wa elimu ya msingi na kuwajumuisha wadau wengine kujadili na kulinda haki ya kila mtoto katika elimu ya msingi.

Timu ya elimu kwa wote iliweza kuomba vibali kwa kupitia wakurugenzi wa manispaa chini ya maafisa elimu. Timu ya elimu kwa wote ilifanya mikutano minne katika shule tofauti hapa Dar es Salaam. Zikiwemo shule tatu tulizofanya utafiti katika wilaya ya Kinondoni. Mkutano wa kwanza kati ya hizi ulikuwa shule ya msingi Pwani ulioudhuliwa na zaidi ya watu 250 wakiwemo wazazi, walimu na viongozi wa nyumba kumi. Kisha shule ya msingi Tandale ambapo idadi ya washiriki ilikuwa zaidi ya 600 wakiwemo wazazi, walimu na viongozi kutoka serikali ya mtaa. Kisha ukafanyika mkutano mmoja katika wilaya mpya ya Ubungo katika shule ya msingi Milenia ya 3

→

## Yaliyomo...


Elimu kwa wote : Wazazi wanajitoleakwa watoto mao (Mbeya)
Vipimo vya Umasikini : Umeanza rasmi mwezi huu wa sita 2017
Hadithi : Pelagie, natua akima rafiki mpya wa ATD

iliyopo maeneo ya Kimara mwisho ambapo pia jumla ya idadi ya watu walioshiriki ni zaidi 640 wakiwemo wazazi, walimu, viongozi wa serikali ya mtaa na afisa diwani kata.

Hatua iliyofuata ni kuupeleka mradi nje ya Dar es Salaam radha ya matokeo ya utafiti katika mikoa mingine. Mkutano ulifanyika mbeya shule ya msingi Ikulu ambapo idadi ya washiriki walikuwa zaidi 375 wakiwemo wazazi, walimu na wawakilishi wa kamati ya shule.

Mapendekezo yalipokelewa vizuri na kuleta mijadala yenye shauku kubwa kati ya walimu, wazazi na viongozi wa serikali za mitaa na madiwani ambao waliunga mkono moja kwa moja mapendekezo yaliyowakilishwa. Mijadala hii yote iliongozwa na wanachama wa ATD, walimu, watu wanaoishi katika umaskini na wanaharakati wa kudumu wa kujitolea wa ATD.

Kulikuwa na umuhimu mkubwa kwa watu wanaoishi katika umaskini uliokithiri kuedesha mikutano hii katika kuongeza kujiamini na kutambulika kwa juhudi zao na kulinda haki za watoto wanaoishi katika umaskini uliokithiri kuanza na kumaliza shule.

Wazazi wengi sana na walimu walizungumzia sana juu ya suala la mawasiliano na mikutano baina ya wazazi na walimu mashuleni. Kulikuwa na maoni mengi sana juu ya haya mapendekezo 11, 12 na 14.

**Pendekezo 11**
**Kuwepo na mfumo wazi mawasiliano kati ya walimu na wazazi. Mawasiliano yanaweza kuwa kwa njia ya mikutano, simu, barua na kutembeleana.**

**Pendekezo 12**
**Kujenga uaminifu na kuboresha mahusiano, washika dau wote wa elimu wanapaswa kuendeleza kutambua kuheshimiana kuhusu hali za wengine.**

**Pendekezo 14**
**Mikutano ya shule iandaliwe na walimu wakuu na wawakilishi wa wazazi. Mikutano iwe ni sehemu ya wazi na walimu kubadilishana uzoefu na changamoto wanazukutana nazo na kulenga zaidi maendeleo ya watoto. Ni muhimu kwamba mawazo ya wazazi yasikilizwe.**

Maoni ya wazazi na walimu……..

“Mikutano ya shule itasaidia kutatua changamoto mbali mbali zinazokabili elimu ya mtoto na pia itaweka ukaribu kati ya wazazi na walimu” mwalimu mkuu

Pia mzazi mmoja alikuwa na cha kuongezea juu ya pendekezo hilo hilo alisema, “Ni muhimu walimu na wazazi kukutana na kuwepo na mawasiliano ya mara kwa mara ili kujua matatizo, mienendo na maendeleo ya wtoto wetu.”

Pia kwa upande wa Dar es Salaam baadhi ya wana timu ya Elimu kwa wote walifanya mkutano mmoja na mwakilishi wa Afisa elimu wilaya ya Ilala katika ofisi yake kwa lengo la kusambaza matokeo ya utafiti, alikuwa na haya ya kusema juu ya mapendekezo.

“Elimu ni dhana ya maendeleo na maendeleo endelevu ni yale yanayofanywa na watu kwa pamoja. Tuondoshe matabaka ya kuwa mimi nina elimu na wewe hauna, tukifanya hivyo itakuwa njia sahihi ya kufikia maendeleo. Matokeo haya ya utafiti ni dhana nyingine imeongezwa katika utendaji wa kazi katika sehemu zote zinazo lega lega katika sekta ya elimu itaweza kukazia.”

Katika harakati za kusambaza matokeo ya utafiti timu ya elimu kwa wote iliweza kufanya mahojiano na mzazi mmoja kutoka Tegeta ambaye ni mmoja wa wajumbe wa kamati ya shule moja shule zilizopo katika eneo la Tegeta na alitueleza. “ Wazazi na walimu tulipokea matokeo ya utafiti kwa furaha sana katika jamii yetu, yaliweza kufungua akili na kufahamu vitu vingi sana, kama kuboresha uhusiano kati ya walimu na wazazi na juu ya adhabu za vitendo kwa watoto namna inavyoaathiri elimu yao endapo mwalimu ataingia na fimbo darasani hupelekea hofu kwa watoto na kushindwa kujifunza vizuri kama tulivyoona katika mapendekezo.

**Pendekezo 10**
**Adhabu za vitendo kwa watoto lazima zitokomezwe. Wazazi na walimu wanapaswa kukubaliana ni aina gani ya adhabu zisizo umiza mwili zitumike.**

***Elimu ni dhana ya maendeleo na maendeleo endelevu ni yale yanayofanywa na watu kwa pamoja. Tuondoshe matabaka ya kuwa mimi nina elimu na wewe hauna, tukifanya hivyo itakuwa njia sahihi ya kufikia maendeleo.***

Katika kusambaza matokeo ya utafiti timu ya elimu kwa wote itaendelea na mchakato huu kwa kipindi hiki cha mwaka mzima na kwa matarajio ya kufanya mikutano mingine miwili nje ya mkoa wa Dar es Salaam ikiwemo Moshi na Njombe. Mikutano mingine na walimu wakuu wa shule za msingi za serikali katika wilaya ya Kinondoni na mikutano mingine katika shule za msingi ndani ya Dar es salaam na kufanya mikutano na afisa elimu wilaya ya Temeke.

# Utafiti wa kipimo cha umasikini umezinduliwa rasmi nchini Tanzania!

Baada ya Mradi wa Elimu kwa Wote, ATD Dunia ya Nne Tanzania inajihusisha katika utafiti wa kimataifa juu ya kubaini vipimo vya umaskini na jinsi ya kuvipima. Utafiti huu unafanywa na ATD Dunia ya Nne ikishirikiana na Chuo Kikuu cha Oxford cha (Uingereza).Mradi huu unahusisha Nchi saba: Tanzania, Bangladesh, Bolivia, USA, Ufaransa, Ukrania na Uingereza. Mradi huu unatarajia kuchukua kipindi cha miaka miwili kufikia matokeo ya mwisho.

Lengo ni kupata ufafanuzi wa kawaida wa umasikini, vipimo vyake mbalimbali na mahusiano kati ya hivyo vipimo. Huu ni mchakato mrefu ambao unahusisha watu tofauti wa asili na uzoefu mbalimbali: watu wenye uzoefu wa moja kwa moja wa umasikini, na watu wenye ujuzi wa umasikini, ikiwa ni pamoja na wasomi, wataalamu, na watunga sera.

Mradi huu umeratibiwa na uliundwa na timu ya mchanganyiko: watu wenye uzoefu wa moja kwa moja wa umasikini, wasomi, wataalamu na wafanya kazi wa kudumu wa kujitolea wa ATD. Kupitia Njia ya kuunganisha Maarifa (MoK) mchakato wa watu wenye uzoefu wa moja kwa moja wa umaskini hutambuliwa kama watafiti wenza, kwa usawa na wengine.

Ni uzoefu wa kushangaza! Tunatarajia kufikia watu tofauti: Wazee, watu wenye umri wa kufanya kazi, vijana, watoto, na makundi maalum ya watu wengine ili kupata uzoefu tofauti wa maisha.

Kwa kufanya kazi katika makundi rika wanajenga aina tofauti za ujuzi: Hatimaye, vipimo vya umaskini vinatambuliwa, vinaelezwa na vinawekwa kulingana na umuhimu na mahusiano.

Tunategemea kufikia makundi ya watu katika mikoa kumi ya Tanzania Bara. Tumeanza na Dar Es Salaam, Kinondoni na Wilaya ya Ilala. Ufikiaji watu umefanikiwa kwa kiasi kikubwa na ushiriki mkubwa wa wanaharakati. Walitutambulisha kwenye serikali za mitaa, kutusaidia kuwabaini watu na kuwasajili ili kuwasiliana nao, na kuwezesha mikutano ya makundi rika.

Mradi huu ni uzoefu mkubwa Ushirikiano wa ATD Dunia ya Nne Tanzania.

## 2017 Wito kwa Kampeni ya kuchukua Hatua

**Saini na ungana na maelfu ya watu**

http://urlz.fr/5r2k

Toa sauti yako ,acha ushuhuda wako. Uliza wanaokuzunguka wanachama wengine wa ATD Dunia ya Nne, shirikiana na familia yako, marafiki, majirani kujiunga na wito wa kuchukua hatua.

ATD FOURTH WORLD
STOP POVERTY
ALL TOGETHER IN DIGNITY



**Timu ya Utafiti ya kubaini vipimo vya Umasikini ilifundishwa kuandaa hatua za kufanya utafiti huko Mbagala (Dar es Salaam)**



Mr. Kasiani, mshiriki wa Timu ya Utafiti wa kubaini vipimo vya Umasikini

Mradi huu unanipa nafasi ya kujifunza zaidi na kuwa na mtazamo tofauti kabisa wa mambo. Jukumu langu kuu ni kumsaidia msimamizi katika uwezeshaji kwenye makundi rika kama makundi ya wazee , watu wazima na kadhalika.

Nadhani mradi utabadili mambo mengi, itabadilisha tabia ya watu kwa sababu watu walikuwa wakifikiria hali yao wenyewe, si hali ya wengine. Mradi huu utasaidia kuelewa nini maana halisi ya umasikini na kufanya kazi pamoja ili kutambua ni nini changamoto.

Katika siku za nyuma, nimekutana na changamoto nyingi, kwa sababu nilikuwa nikifanya mambo tofauti katika jamii yangu kama vile kusaidia watu kusoma na kuandika katika darasa la watu wazima.
Ninaweza kusema kwamba baadhi ya majirani walikuwa wakicheka juu yangu, walifikiri nilikuwa napoteza muda wangu lakini leo wameanza kubadilika kwa sababu wakati mwingine wanakuja kuniona na kuuliza maswali juu ya kujiunga na sisi katika ATD.

Katika siku hizi tatu za makundi rika huko Kunduchi (Bw. Kasiani alikuwa katika kikundi cha wazee) mwanzoni tulianza kwa mtazamo kutoka kwetu wenyewe na kisha tulishirikishana uzoefu wetu ili kuzalisha ufahamu wa kawaida.

Nadhani mradi huu utaendelea kuwa wa nguvu, kwa sababu tumepewa mafunzo kwenye mradi na tunatumia kile tunachojifunza kutokana na mafunzo kwa wengine, lakini mafunzo hayatoshi.

# "Ninaona kama tukiendelea kuwa pamoja nao inaleta matumaini ya baadaye."



Katika mapambano yanayoongozwa na wanachama wa ATD dunia ya nne, tuna nafasi ya kukutana na marafiki wapya ambao wamegundua moyo wa kujitoa na kupata njia inayooana na malengo yetu.

Pelagia kutoka Rwanda anaishi hapa Dar es Salaam, Tanzania tangu mwaka 2009 pamoja na familia yake. Mwaka uliopita aligundua shirirka la ATD dunia ya nne. Mara alijihusisha na watoto wa maktaba ya mtaa Tandale na wakati mwingine anasaidia timu kama vile kutafsiri. Kwa sasa anajihusisha kwa nguvu zote na mradi wa utafiti wa kubaini vipimo vya umaskini na njinsi ya kuvipima.

Kitu fulani kilifanya kuvutiwa na ATD. Nimeijua ATD tangu mwaka uliopita lakini kabla sikuona shirika ambalo watu wanoishi katika umaskini wanaheshimiwa na kupewa haki ya kufikiri na kupanga pamoja na watu wengine wasioishi katika umaskini. Nilicho kigundua katika ATD ni kitu cha peke: Ni kweli watu wanoishi katika umaskini wanaheshimiwa. Wanachama wa ATD wanajaribu kwa kiasi kikubwa kuonyesha utu kwa watu maskini. Hili kweli limeugusa moyo wangu, na mimi nikasema kwa nini nisijiunge na hawa watu kutoa mchango wangu kwa kuendeleza utu wa binadamu? Kwa sababu watu wanoishi katika umaskini ni binadamu kama wengine, hivyo hawana budi kuheshimiwa na kupata haki zote za binadamu.

Nilianza kwa moyo kushiriki katika shughuli za maktaba ya mtaa kwa sababu inanipa matuamini kwamba maisha ya hawa watoto yatakuwa mazuri. Ninapowaona wanakuja na kushirikiana kwa pamoja kusoma vitabu na kusikiliza hadithi, ninaona kama tukiendelea kuwa pamoja nao inaleta matumaini ya baadaye.

Pelagia mara kwa mara matumaini yake nikuona hii heshima inatolewa kwa kila kundi kwenye jamii na kwa kila binadamu na hasa wanoishi katika umaskini uliokithiri. Pelagia anasema kwamba mtazamo wa wanachama wa ATD juu ya watu maskini unapaswa kuwa mfano mzuri kwa mashirika mengine yanayojihusisha na maswala ya umaskini.

Niliona kwamba hakuna kitu kizuri kuliko kukaa na watu maskini na kuwawezesha kupanga kwa ajili yao, kuandaa mipango ya maendeleo yao binafsi. Ninafikiri mambo mengi yanafeli kwa sababu hakuna anayejihusisha kujua kwa upana zaidi hasa mahitaji ya walengwa.

Katika mradi wa kubaini vipimo vya umaskini, ninapowasikiliza watu maskini wanavyotoa mawazo yao inanifanya kuamini kwamba watu wanaoishi katika umaskini wanaelewa umaskini ni nini, na pia wanaelewa nini kifanyike kuondokana na umaskini.

Hata hivyo , baada ya mwaka mmoja nimeona kitu kikubwa katika ATD ambacho sio rahisi kuelewa kwa muda mfupi: falsafa ya ATD, bado ninahitaji kuelewa zaidi. Hivyo niko tayari kujitoa kwa moyo wote kuijua ATD ili niweze kutoa mchango wangu.


ATD Dunia ya Nne - SLP 61786 - Dar es Salaam
Namba ya Ofisi: 0222761717
atd.tanzania@gmail.com
Kiswahili website: http://www.atd-fourthworld.org/where-we-are/africa/tanzania/tanzania/
Ukurasa wa Facebook: https://www.facebook.com/atd.duniayanne